JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mtaa wa Mkoani,
S.L.P 273,
55103 RUKWA,
Barua pepe: rbcrukwa@pccb.go.tz,
TANZANIA.

RUKWA AGOSTI, 2022

TAKUKURU RUKWA YAFUATILIA UTEKELEZAJI WA MIRADI SABA

Ndugu Wanahabari,
Katika kipindi cha Mwezi Aprili hadi Juni, 2022, TAKUKURU Mkoa wa Rukwa imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007 kupitia madawati ya Uzuiaji Rushwa, Elimu kwa Umma pamoja na Uchunguzi na Mashtaka.

UZUIAJI RUSHWA
Ndugu Wanahabari,

Ili kuboresha mifumo mbalimbali ya utoaji wa huduma kwa wananchi, katika kipindi hiki TAKUKURU Mkoa wa Rukwa iliendelea kufanya chambuzi mbalimbali za **mifumo mbili (2)** ikiwemo Uchambuzi wa mfumo wa tathmini ya utendaji kazi wa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) Manispaa ya Sumbawanga na uchambuzi wa mfumo wa mianya ya rushwa katika Sheria ndogo ndogo za Afya na Mazingira - Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo. **Yaliyobainika ni yafuatayo:**

Katika Uchambuzi wa mfumo wa tathmini ya utendaji kazi wa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) Manispaa ya Sumbawanga ilibanika kuwa:-

- Asilimia 65 ya taasisi za Serikali ambapo zinapaswa kufanya manunuzi yao GPSA zilieleza kuwa bidhaa hazipatikani kwa wakati hivyo kulazimika kununua kwa wazabuni wengine waliopendekezwa na GPSA, na
- Asilimia 35 ya taasisi za Serikali zilidai kuwa bidhaa zinapatikana kwa wakati.
- Ushauri uliotolewa ni kuwa GPSA waboreshe mfumo wa udhibiti wa hesabu ya orodha ya vifaa katika stoo zao (inventory control system) ili kuhakikisha hawaishiwi bidhaa na wanatoa huduma kwa wakati.

Katika uchambuzi wa mianya ya Rushwa kwenye Sheria ndogo ndogo za Afya na Mazingira - Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ilibanika kuwa:-

- Wananchi wana uelewa mdogo sana wa sheria hizi jambo linalosababisha wanapotozwa faini wanahisi wanaombwa Rushwa. Hivyo iliazimiwa kuwa elimu iendelee kutolewa juu ya sheria hizi zinazohusu Afya na Mazingira kwa wananchi.

UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Aidha, katika kipindi hiki, tumefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa **miradi saba (7)** ya ujenzi yenye thamani ya shs. **3,193,370,233.47** ili kujua kama kweli fedha iliyotumika inalingana na kazi iliyofanyika.

TAARIFA YA MIRADI ILIYOTEMBELEWA

NA	JINA LA MRADI	ENEO LA MRADI	KIASI CHA FEDHA
1	Ujenzi wa Mradi wa maji kijiji cha Msanda Muungano	Kata ya Msanda Muungano, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga	295,762,712.50
2	Ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi VETA,	Kata ya Sumbawanga, Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga	2,035,364,881.97
3	Ujenzi wa Mradi wa maji kijiji cha Chala	Kata ya Chala, Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi	164,742,639/=
4	Ujenzi wa mradi wa Chumba cha Dharura (ICU) Hospitali ya Wilaya ya Nkasi	Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi	300,000,000/=

5	Ujenzi wa mradi wa Chumba cha Dharura (ICU) Hospitali ya Wilaya ya Kalambo	Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo	250,000,000/=
6	Ujenzi wa umaliziaji wa vyumba vitatu vya madarasa Shule ya Sekondari Mkali	Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo	57,500,000/=
7	Ujenzi wa nyumba ya watumishi (3 in 1) Hospitali ya Wilaya ya Kalambo	Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo	90,000,000/=
JUMLA			**3,193,370,233.47**

Katika zoezi la kutembelea miradi hii, ilibainika kuwa, baadhi ya miradi hasa ile inayotekelezwa kwa utaratibu wa "*Force Account*", baadhi ya Wajumbe wa Kamati simamizi za miradi hawana uelewa wa kutosha kuhusu Sheria ya Manunuzi ya Umma, hivyo ushauri ulitolewa kwa Wanakamati hao kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo kwa kushirikiana na Wataalam wa Halmashauri za Wilaya.

Aidha TAKUKURU Mkoa wa Rukwa imetoa ushauri kwa Mafundi na Wakandarasi wanaoendelea na ujenzi wa miradi, kukamilisha miradi hiyo kwa wakati ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria pindi watakapo shindwa kuikamilisha miradi hiyo kwa wakati kwa mujibu wa mikataba.

ELIMU KWA UMMA

Ndugu Wanahabari,

Katika kuhakikisha kwamba Wananchi wa Rika na Kada mbalimbali katika Mkoa wa Rukwa wanaendelea kupewa elimu na uelewa juu ya vitendo vya Rushwa ili washiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya Rushwa ndani ya jamii yetu, TAKUKURU Mkoa wa Rukwa imeendelea na uelimishaji kama ifuatavyo:-

Na.	Kazi	Ufafanuzi
1.	Jumla ya Semina 6 makambini na mashuleni, kwa kushirikiana na Chama cha Skauti chini ya mpango wa TAKUSKA zimefanyika.	Haya ni mafunzo ya kukuza uzalendo, uwajibikaji na maadili kwa vijana kama nyenzo muhimu ya kujenga kizazi kinachochukia rushwa.

2.	Jumla ya mikutano 10 imefanyika ikiwemo mitatu (3) ya *Programu* ya *TAKUKURU INAYOTEMBEA* (*PCCB MOBILE*).	Kutoa msisitizo wa wananchi kushiriki katika mapambano dhidi ya Rushwa kupitia mikutano ya hadhara.
3.	Klabu za Wapinga Rushwa 25 za Shule za Msingi na Sekondari zimetembelewa. - Vijana wanaendelea kukua kimaadili ili kuwa na kizazi kinachochukia Rushwa	Kutembelea na kuziimarisha Klabu za Wapinga Rushwa katika Shule za Msingi na Sekondari.
4.	Jumla ya makala nne (4) zenye maudhui ya mapambano dhidi ya Rushwa zimeandikwa.	Uandishi wa makala kama nyenzo nyingine ya kufikisha elimu kwa makundi mbalimbali
5.	Semina 11 zimefanyika kwa wadau mbalimbali wajumbe wa kamati simamizi za miradi inayotekelezwa kwa mfumo wa *Force Account.*	Kuongeza uelewa wa makosa ya Rushwa na madhara ya Rushwa kwa makundi mbalimbali kupitia semina.
6.	Mkutano mmoja (1) na wanahabari umefanyika. Lengo likiwa ni kufikisha elimu hii sehemu mbalimbali ndani na nje ya Mkoa wa Rukwa.	Kutumia vyombo vya habari kufikisha elimu ya mapambano dhidi ya Rushwa kwa jamii.

UCHUNGUZI NA MASHTAKA

(i) Taarifa zilizopokelewa (Kisekta).

Katika kipindi hiki, TAKUKURU Mkoa wa Rukwa imepokea jumla ya **taarifa 45;** kati ya hizo, taarifa 25 zilihusu rushwa ambapo ofisi inaendelea kuzifanyia kazi na uchunguzi wake unaendelea.

Taarifa 20 kati ya 45 zilizopokelewa hazikuhusu rushwa, hivyo ofisi imetoa ushauri kwa watoa taarifa na kuwaelekeza mahali sahihi pa kuwasilisha malalamiko hayo na hakukuwa na taarifa iliyohamishiwa idara nyingine. Mchanganuo wa taarifa 45 zilizopokelewa KiSekta ni kama ifuatavyo:

IDARA/SEKTA	SUMBAWANGA	KALAMBO	NKASI	JUMLA
Tamisemi	6	0	1	7
Binafsi	5	0	0	5
Afya	3	1	1	5
Polisi	2	0	1	3
Baraza la Kata	5	1	2	8
Mahakama	2	1	2	5
Siasa	0	1	0	1
S/Vijiji	2	2	2	6
TANESCO	1	0	0	1
Elimu	0	1	0	1
Biashara	0	0	1	1
Mawasiliano	0	0	1	1
M/Jamii	0	0	1	1
JUMLA KUU	**26**	**7**	**12**	**45**

(i) Kesi zilizoendelea Mahakamani.

Katika kipindi hiki, TAKUKURU Mkoa wa Rukwa imefungua kesi sita (6) Mahakamani na hivyo kuufanya Mkoa wa Rukwa kuwa na jumla ya kesi **kumi na moja (11)** zinaendelea katika Mahakama mbalimbali mkoani humu. Katika kipindi husika, kesi mbili (2) zilitolewa maamuzi ambapo zote Jamhuri ilishinda.

Ndugu wanahabari

Zoezi la ufuatiliaji wa wadaiwa sugu (*Defaulters*) wa ukusanyaji wa fedha za Halmashauri za Wilaya katika Mkoa wa Rukwa kwa waliokabidhiwa mashine za kukusanyia mapato (POS) limeendelea kufanyiwa uchunguzi katika Kipindi husika. Na katika uchunguzi huo imebainika ni kweli kuna upotevu wa fedha katika ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mashine za POS, hivyo TAKUKURU Mkoa wa Rukwa ipo hatua za mwisho za kukamilisha uchunguzi ili majalada ya uchunguzi huo yapelekwe Ofisi ya Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Rukwa kwa ajili ya kuomba kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani.

MIKAKATI YA MWEZI JULAI HADI SEPTEMBA, 2022:

TAKUKURU Mkoa wa Rukwa kupitia Dawati la Uzuaji Rushwa itaendelea kufanya ufuatiliaji wa fedha zinazotolewa na Serikali katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo hasa ile inayoendelea kutekelezwa kwa

utaratibu wa *"Force Account"* katika Halmashauri za Wilaya kwa lengo la kuziba mianya ya rushwa na kudhibiti upoteaji wa fedha za Serikali katika utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na kufuatilia Miradi ya Ujenzi wa barabara zilizo chini ya TARURA.

TAKUKURU Mkoa wa Rukwa itaendelea pia kufanya udhibiti na uchunguzi kuhusu ubadhirifu wa fedha za Serikali katika ugavi wa dawa na bidhaa za afya (vifaa tiba), ambao umekuwa ukijitokeza katika Vituo vya Afya na Hospitali za Serikali Mkoa wa Rukwa ili wote wanaohusika na ubadhirifu huo wachukuliwe hatua za kisheria.

Aidha, kwa upande wa Uelimishaji Umma tutaendelea na uelimishaji huku msisitizo mkubwa ukiwa katika kuendeleza ushirikiano kupitia TAKUKURU na SKAUTI kwa kutekeleza kazi zilizoainishwa katika Mpango Kazi wa Ushirikiano kwa kuwalenga vijana.

Kwa upande wa Uchunguzi na Mashtaka, TAKUKURU Mkoa wa Rukwa inakusudia kufikisha Majalada sita (6) Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ili kupata Vibali vya kuyafikisha watuhumiwa Mahakamani.

WITO:

Ndugu Wanahabari,

TAKUKURU Mkoa wa Rukwa bado inaendelea kutoa rai kwa wale wote wanao watapeli wananchi kwa kujifanya maafisa wa TAKUKURU na wale wanaoendelea kujihusisha na vitendo vya rushwa waache mara moja, kwani wakikamatwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

TAKUKURU Mkoa wa Rukwa tunaendelea kutoa shukrani kwa viongozi mbalimbali na wananchi kwa kuendelea kuunga mkono mapambano dhidi ya rushwa kwa kutoa taarifa zinazohusu vitendo vya rushwa.

Aidha, tunawashukuru sana wanahabari wote katika Mkoa wetu wa Rukwa ambao mmekuwa mstari wa mbele kufikisha elimu hii ya mapambano dhidi ya rushwa kwa wananchi wa mkoa wa Rukwa na maeneo mengine, maana jukumu la mapambano dhidi ya rushwa si la TAKUKURU pekee bali linamhusu kila mtu na kila mtanzania.

Imetolewa na:

THOMAS MSUTA,
KNY: MKUU WA TAKUKURU (M) RUKWA
SIMU: 0738150186

Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022